

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIUNDOBINU

Telegrams: MIUNDOBINU, DAR ES SALAAM
SIMU: 255 22 2112857
FAX: 255 22 2112751
E-Mail: wzuj@africaonline.co.tz
Kumb. Na. MI/PRV/SEC/2006/232



S.L.P. 9144
DAR ES SALAAM

27/02/2007

Mwenyekiti,
Umma wa Wapanda Baiskeli,
UWABA
S.L.P. 12247,
Dar es Salaam.

**YAH: OMBI LA UONGOZI WA UWABA KUKUTANA NA WAZIRI WA
MIUNDOBINU.**

Tafadhali, barua yako ya tarehe 18/02/2007 inahusika.

Mhe. Andrew J. Chenge (Mb.), Waziri wa Miundombinu anapenda kuthibitisha kupokea barua yako tajwa hapo juu ambayo iliwasilisha rasmi ombi la UWADA kufaka kuonana naye.

Kimsingi, Mhe. Waziri amefiki haja ya kupanga kuwapo kwa kikao cha pamoja. Hatua hiyo inatokana na yeye kuunga mkono azma yenu ya kuunda asasi hii muhimu ya wapanda baiskeli hasa kama mlivyoetezea kwa nia ya kutunzaji wa mazingira, kupunguza msongamano wa magari mijini, kupunguza gharama za usafiri na pia kama chombo muhimu kwa mazoezi.

Katika hali hii na kwa kuzingatia kuwa bado wapo wadau wengine wengi wa kufanya mashauriano nao zikiwemo taasisi kadhaa chini ya Wizara ya Miundombinu kama vile Tanroads, Kitengo cha Usalama Barabara pamoja na SUMATRA, itakuwa muafaka kukutana na Mhe. Waziri baada ya kujiridhisha kuwa kuna uelewa wa pamoja kwa vyombo vyote hivi kuhusiana na azma hii.

Nakutakia shughuli njema,

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Martin Ntemo'.

Martin Ntemo
Katibu wa Waziri

Nakala: NW1
NW2
KM